**Utapata mavuno gani ukitumia mbolea?**

- Ukitumia samadi utapata zaidi ya magunia 30 kwa ekari moja.
- Ukitumia urea utapata zaidi ya magunia 40 kwa ekari



Mavuno ya mpunga

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:


Mkurugenzi wa Kanda
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Ukiriguru
S.L.P. 1433
Mwanza.
Simu: 028 2550215
Fax: 028 2550214
E-mail: ukiriguru@africaonline.co.tz


Kipeperushi hiki kimetayarishwa na Taasisi ya Kilimo Ukiriguru na kimefadhiliwa na Serikali ya Tanzania na Uholanzi

LZARDI
Lake Zone Agricultural Research & Development Institute

Kipeperushi hiki hakiuzwi.

UL 19

24

# Pata mavuno mengi ya mpunga kwa kutumia mbolea.



Kweli mpunga uliowekewa mbolea unazaa sana

**Utangulizi.**
Matumizi ya mbolea kama vile samadi na urea huongeza mavuno ya mpunga. Inashauriwa kutumia mikokoteni tatu au zaidi kwa ekari kila baada ya miaka mitatu, na vilevile kutumia makopo ya kimbo ishirini na sita kwa ekari na mavuno yatongezeka kwa asilimia kumi na tano mpaka thelasini na mbili (15%-32%).Na usipoweka bolea kwenye shamba lako matokeo yake shamba uchoka na mavuno kupungua au kukosa kabisa.

**Wakati gani mbolea iwekwe shambani?**

- **Samadi** itawanywe shambani kabla ya kukatua au kulima kwa jembe la ng'ombe.
- Vuruga au changanya mbolea na udongo kabla ya kupandikiza mpunga.
- Pandikiza mpunga wako katika nafasi ya sentimita 20 kwa 20.
- **Urea** iwekwe mwezi mmoja baada ya kupunguzia miche ya mpunga.
- Hakikisha mbolea yako haimwagikiwi na maji.
- Magugu yaondolewe kabla ya kuweka mbolea ili yasitumie mbolea hiyo.



**Faida za matumizi ya mbolea kwenye mpunga ni zipi?**

- Mavuno huongezeka kwa zaidi ya asilimia kumi na tano.
- Mabua na masalio ya mpunga huongezeka.
- Ng'ombe na mifugo mingine hupata chakula cha kutosha.

**Jinsi ya kuweka mbolea kwenye shamba la mpunga.**

- Weka mbolea wakati udongo una unyevu wa kutosha.
- Hakikisha kina cha maji ni kati ya sentimeta 1 na 15.
- Baada ya kuweka mbolea maji yabakie jarubani muda wa mwezi mmoja.
- Mbolea iwekwe shambani kwa njia ya kusia.




**Utaweka kiasi gani cha mbolea shambani?**

- Weka samadi mikokoteni mitatu au zaidi kwa ekari moja.
- Kila baada ya miaka mitatu weka upya samadi shambani.
- Weka urea makopo ya kimbo 26 kwa ekari
- Weka urea makopo ya kimbo13 kwa nusu ekari
- Weka urea makopo ya kimbo 7 kwa nusu ekari.

